Pambazuko

Toleo Namba 069 Jumatatu Aprili 15-21, 2024

# Je, Watanzania wako salama?

- *Ni endapo 'mbu wa kutengenezwa' wataachiwa*



## Lembeli: Nilirudi CCM kwa kumwogopa Rais Magufuli



UK. 11

## Mchakato wa mabadiliko Simba unachosha




UK. 18&19

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Tahariri

## Rais Samia sasa achukue hatua kali

MACHI 29, mwaka jana - 2023, Rais, Samia Suluhu Hassan alionyesha hasira zake kwa umma kwa kutamka maneno makali.

Akipokea ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali (CAG), jijini Dar es Salaam, Rais Samia alikerwa mno na kuwepo kwa kila dalili za rushwa, wizi na ubadhirifu ambazo zimesheheni ndani ya taarifa hiyo aliyokabidhiwa.

Katika uongozi wake uliotimiza miaka mitatu sasa, kwa mara ya kwanza, Watanzania na dunia walishuhudia namna ambavyo Rais Samia hapendi rushwa, wizi na ubadhirifu. Alifoka huku sura yake ikionekana "kuvaa" hasira.

Rais Samia alifika wakati akatumia maneno makali ya Kiingereza; "stupid" – akimaanisha upumbavu mkubwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa wakishindwa kutumia uzalendo kwa kuwajibika, badala yake wamekuwa wakiamini dhamana zao ni chumo lao kwa manufaa binafsi.

Pambazuko tunapongeza hasira hizo za Rais Samia, ingawa bado tunaamini kwamba hasira pekee hazitoshi kuwakemea Watanzania wengi kuacha rushwa, kujihusisha na ubadhirifu na hata matumizi mabaya ya dhamana walizokabidhiwa kwa niaba ya wananchi.

Tunatambua kuwa Rais Samia amekuwa sehemu ya utendaji wa serikali kwa muda mrefu, hivyo tunaamini anatambua wapi kuna mianya mingi ya rushwa, ubadhirifu na uchafu mwingine ambao unachafua taswira ya serikali yake kwa umma wa Watanzania na dunia.

Kimsingi, wanaotenda maovu hayo, wanamchongea Rais Samia kwa wananchi, na kumuonyesha kwamba ni kiongozi asiyechukua hatua kunapotokea uchafu katika utendaji wa serikali.

Kama ambavyo wananchi wengi wanapendekeza Rais Samia kuchukua hatua kali; ikiwamo kuwatimua kazini na kuwafungulia mashtaka wote wanaoiba mali za wananchi, nasi katika Pambazuko tunasisitiza kiongozi huyo wa nchi kuchukua hatua kwa wote wanaomhujumu.

Kuiba mali ya umma ni dhambi kubwa mno, kwani inahusisha kudhulumu haki za idadi kubwa ya wananchi.

Kuiba fedha za maendeleo maana yake ni kwamba mwizi huyo anakwamisha ujenzi wa barabara, anachelewesha kama siyo kuzuia kabisa ununuzi wa dawa katika hospitali na anakwamisha kuimarika kwa elimu ya watoto wetu.

Mwizi wa mali ya umma ni mbaya mno. Ni sawa kabisa na kuua watu kwa manufaa ya mtu binafsi.

Ndiyo maana nchi zingine, mwizi wa mali ya umma hupigwa risasi hadharani ili kuwa fundisho kwa watendaji wengine wenye tamaa ya kupata utajiri wa harakaharaka kwa mgongo wa fedha za maendeleo ya umma.

Pambazuko linamuomba Rais Samia sasa kuwa mkali zaidi kwa wezi na wale wanaotumia vibaya dhamana zao.

Sisi Pambazuko tuko tayari kumsaidia kwa njia tunazoweza ili kuifanya Tanzania ikome kuwa shamba la bibi, ambamo kila anayepita jirani, anakula mazao bila kukemewa.

# Pishi la mke wa rais...




***Mariam Mwinyi, mke wa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, akipika chakula, ikiwa ni ishara ya kuhimiza ulaji wa vyakula unaofaa kwa ajili ya kulinda afya ya mwili na akili. (Picha imepatikana kutoka Mtandao wa X wa Shirika la Chakula Duniani (FAO).***

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



***"Hatuwezi kuendelea kukopa, hatuwezi kuendesha nchi kwa kutumia mikopo, lazima kila mtu alipe ushuru. Katika utawala wangu, hakuna mtu atakwepa ushuru na aendelee kukumbatiwa, lazima alipe na hatua kali zichukuliwe kama atakwepa," – Rais wa Kenya, William Ruto.***

# Tangazo

## Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu, Oktoba, 2023**

## Changia **Pambazuko** liendelee

**WAJUMBE** wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufurahia kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasirimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiswahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokua zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili – miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukuza Kiswahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoa uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kuimarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili lianze kuuzwa, lakini haukubaliani na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapenda kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni michango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

**Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TiGO na utatufikia; 6214500,** Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya **Mpesa: 0744 768 263**

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti.**
Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako – na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263.**

**Lipa kwa Simu**

Lipa kwa kuscan

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

# Wanawake Mererani wamlilia Samia

**Mwandishi WETU,**
**Mererani**

MAISHA ya wanawake "wanaotafuta maisha" kwa kuchekecha mchanga katika machimbo ya Tanzanite, Mererani, Manyara, yako hatarini baada ya "kukatika" kwa kipato chao.

Kipato cha wanawake hao kinatokana na kuwepo kwa mgogoro wa ardhi, hivyo kulazimika kufungwa kwa baadhi ya migodi ya wachimbaji wadogo.

Wachimbaji wadogo wa Mererani wako katika mgogoro wa mipaka na mwekezaji Kampuni ya Franone Mining and Gems.

Kufungwa kwa migodi hiyo kunawafanya kushindwa kumudu maisha na kuendeleza familia, hasa watoto wanaosoma, hivyo wanaomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingia kati, ili kazi zao ziendelee.

Wanawake hao wameliambia Pambazuko kwamba kufungwa kwa migodi hiyo na njia zake, ikiwepo mgodi wa Saniniu Laizer, ambao hadi sasa unashikilia rekodi ya kutoa madini makubwa, lakini pia kulipa kodi kubwa kwa serikali, kumewasababishia umasikini mkubwa.

Helena Daud, mchekechaji wa madini anasema kufungwa Kwa migodi ya wachimbaji wadogo kumesababisha kuwa na hali ngumu zaidi kwao.

Naye Ummy Rajabu Chandu, mchekechaji wa madini anaungana mwenzake Kwa kusema kuwa kufungwa kwa migodi ya wachimbaji wadogo kumeathiri uchumi na ajira za wanawake.

Akizungumzia athari hizo za migodi kufungwa, mfanyabiashara wa madini huko Mererani, Herieth Evarist Mushi anasema wameshindwa kuwapeleka watoto shule baada ya Mji wa Mererani "kufa kwani watu hawana ajira na wamekosa madini kutokana na kufungwa kwa migodi yao.

Lightness Daniel, mkazi wa Mererani anasema kuchukuliwa njia za madini Kwa wachimbaji wadogo kumesababisha



*Wanawake wachekechaji wa mchanga kwenye machimbo ya Mererani wakimuomba Rais Samia kuwasaidia*

kukosekana kwa ajira Kwa watu wengi .

Migodi ya wachimbaji wadogo ambayo imefungwa ndio hutoa fursa ya ajira nyingi kwa vijana na kuwapa udongo wanawake kwa ajili ya kuchekecha.

Wakizungumzia mgogoro wa Mererani, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde ametaka busara kutumika kumaliza migogoro ya mipaka huko Mererani.

Waziri Mavunde anasema serikali haitaki kuona Mererani inakuwa na vurugu lakini pia Kuna wachimbaji wanahujumiana.

Alisema Wizara yake pia imekamilisha zoezi la kupiga picha eneo lote ya Migodi ya Tanzanite ndani ya Ukuta na nje ili kuona akiba ya Madini iliyopo.

Katika machimbo hayo mgogoro mkubwa ni Sheria ya Uchimbaji Madini ya Vito ambayo inataka mchimbaji kuchimba madini katika eneo lake la leseni tu kwenda chini.

Hata hivyo, wachimbaji wanapinga sheria hiyo kwani Madini ya Tanzanite wanachimba kwa kufuata miamba ya madini na mingi inaelekea kitalu C ambacho amepewa mwekezaji mmoja tu, Kampuni ya Franone .

Katika machimbo ya Mererani kuna zaidi ya migodi 400 katika kitalu A,B,D lakini kitalu C Kuna wekezaji mmoja tu wa Kampuni ya Franone.

# Habari

## Je, Watanzania wako salama?

**Na Mwandishi MAALUM**

MAMILIONI ya mbu wanaozalishwa maabara, wako mbioni "kuachiwa huru" ili kuingia "mitaani" kwa lengo la kuwauma, na ikiwezekana, kuwaua mbu wanaosambaza malaria nchini Tanzania.

Inadaiwa kuwa mbu hao wanaozalishwa katika maabara za Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), yenye vituo vya maabara kadhaa Tanzania, "wametengenezwa" kwa kupandikizwa jene ambazo hazina madhara kwa binadamu hata kama watamng'ata.

Pambazuko limeshindwa kuthibitishiwa ni lini hasa mamilioni hayo ya mbu yataachiwa huru ili kuanza kazi ya kuua mbu wengine wenye madhara kwa binadamu. Pia haikufahamika mara moja maeneo ambako mbu hao wenye uwezo wa kuua wenzao, watasambazwa.

"Siwezi kuthibitisha wala kueleza wapi na lini mbu hao wataachiwa kwa ajili ya majaribio, na ieleweke hapa Ifakara, tunafanya majaribio ya kisayansi na hatuwezi kufanya jambo au utafiti ambao utakuwa na madhara kwa watu," amesema mtendaji mmoja wa taasisi hiyo, huku akikataa kutajwa jina.

Pambazuko limeona baadhi ya maandishi ndani ya taasisi hiyo kuwa mbu hao wataachiwa hivi karibuni, baada ya kukamilika kwa hatua za kuwazalisha ndani ya maabara.

Inaelezwa na vyanzo kadhaa vya habari kuwa Tanzania, kupitia Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI), hivi sasa iko katika hatua ya pili ya majaribio ya kimaabara ambapo mbu waliotengenezwa wanahifadhiwa kwenye matundu makubwa kwa ajili ya kupima matokeo ya awali.

Baadaye katika hatua ya tatu, mbu hao wataachiliwa huru kwa kiasi fulani, kabla ya kuachiliwa kwa wingi kwenye hatua ya nne ili wafanye kazi yao – ya kuwala mbu wa asili.

Hata hivyo, kuna taarifa ambazo Pambazuko limesikia ni kuwa siyo waendeshaji wa mradi huo nchini - Ifakara Health Institute na hata Serikali ya Tanzania iliyochukua hatua zozote kwa kufanya upembuzi yakinifu kwa hatua ya kuachiwa kwa 'mbu hao wapya.'



*Ummy Mwalimu - Waziri wa Afya*

Dkt. Dickson Wilson Lwetoijera, daktari bingwa wa magonjwa ya kitropiki yanayosambazwa na wadudu wa IHI, amesema kuwa taasisi yake kweli inazalisha mbu wa "kutokomeza malaria" kwa kuwaua mbu wengine wa asili.

Mtafiti huyo wa IHI, amekanusha kuwa kuna mamilioni ya mbu wataachiwa ili wakaue wenzao wanaosambaza malaria, isipokuwa mbu wanaozalishwa hubaki ndani ya maeneo maalum, hasa ya utafiti ndani ya viwanja vya taasisi hiyo.

Bingwa huyo wa utafiti wa magonjwa ya kitropiki, anasema mara nyingi mbu hao wanakunywa damu ya ng'ombe, na kwamba IHI hupeleka kundi la ng'ombe au kuchukua damu yao kisha kuiingiza katika mifumo maalumu isigande kisha kuwa chakula cha mbu.

Dkt. Lwetoijera amesema kamwe serikali haiwezi kuruhusu watu wake, wakafanyiwa majaribio yenye madhara na kwamba kuja kwa mradi huo kulipitia mchakato mrefu na kuna uhakika wa kutoleta madhara.

Mpaka sasa watafiti wa mradi kama wa IHI, katika nchi za Burkina Faso, Uganda na Ghana wameshindwa kutoa maelezo ya kutosha juu ya namna mbu wapya watakuwa na uwezo wa kumaliza wale

*Inaendelea Uk. 7*

# Je, Watanzania wako salama?

*Inatoka Uk. 6*

wenye vimelea vya malaria.

HIVI karibuni kulizuka gumzo kubwa kuhusu usalama wa vyakula vinavyoingizwa nchini kutoka nje.

Watanzania wengi kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii wakaanza kuhoji uwajibikaji wa serikali na hasa taasisi na mashirika yanayohusika kudhibiti ubora wa vyakula na bidhaa nchini.

Haya yalitokea baada ya kusambaa kwa taarifa za kuingizwa kwa msaada wa mchele na mafuta ya kula kutoka Marekani. Msaada uliolenga kufaidisha shule zaidi ya 350 chini ya mapango wa 'Pamoja Tuwalishe' ('Together Let's Feed Them').

Tanzania, imekuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika ambazo zinapata "fursa" ya kuwa eneo la kufanyia majaribio ya mambo kadhaa kupitia miradi ya afya, elimu, kilimo na mengine.

Ni katika mchakato wa miradi hiyo, baadhi ya matokeo yake hubainika baadaye kuwa na madhara, hali ambayo ingetambuliwa mapema, ingeweza kuokoa madhila.

Ipo baadhi ya miradi ambayo imekuwa ikiendeshwa nchini Tanzania, na hakuna kelele zinazopigwa, huenda kwa kuwa kuna usiri mkubwa wa kile kinachofanywa na miradi hiyo.

Leo Pambazuko linaanza na mradi wa uzalishaji mbu wa vinasaba, je, Watanzania wanautambua? Wako salama kiasi gani kwa wadudu hao endapo wataachiwa? Nani anawadhibiti endapo wataanza kuachiwa, nini madhara yake?

Mradi huu unaojulikana kama "Transmission Zero" ulianzishwa na Mpango wa Utafiti wa Ugonjwa wa Malaria Duniani (Global Malaria Research Programe) kwa lengo la kupambana na ugonjwa wa malaria Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kinachofanyika katika mradi huu ni "kutengeneza" mbu wa kibaiolojia kwa kubadilisha vinasaba vyao vya asili



*Mbu*

kwenda hali mpya kwa kubadilishwa vinasaba.

Kwa kawaida vinasaba vya viumbe hai vina asilimia ya kuweza kurithiwa na watoto, lakini kwa kufanya 'gene drive' upo uwezekano huo hupanda kufikia asilimia 99. Hii ina maana wajukuu wa mbu watakaozalishwa chini ya mpango huu watakuwa na vinasaba vipya kabisa.

Kwa mujibu wa taarifa za waandaaji wa mpango huu, mbu wapya watakaozalishwa watakuwa na uwezo wa kuwauma na kuwaua mbu aina ya anopheles wanaoambukiza ugonjwa wa malaria.

Kwa hiyo, baada ya miezi au miaka kadhaa ya kusambazwa kwa 'mbu wapya,' mbu wanaoishi sasa – wakiwamo wanaosambaza malaria, watapungua zaidi ama kutoweka kabisa, maana watauawa.

Ikiangaliwa kwa haraka, inaonekana kuwa mradi huu ni wenye manufaa zaidi, kwani inadaiwa kuwa utamaliza ugonjwa wa malaria unaoua mamilioni ya watu kila mwaka.

Mradi huu ni kificho kwa mradi mwingine?

Mojawapo ya sifa kubwa ya nchi zilizoendelea, ni kutumia hadaa na ulaghai wa kijasusi katika kufanikisha mipango yao.

Ndiyo maana inapaswa Watanzania kujiuliza mara kadhaa endapo lengo la mradi huu ni kupambana na malaria kweli au kuna lingine?

Je, serikali ina uwezo na utaalam

*Inaendelea Uk. 8*

# Habari

## Je, Watanzania wako salama?

*Inatoka Uk. 7*

wa kubaini mbinu, hujuma au uharibifu wowote (kama upo) unaoweza kutengenezwa kupitia mradi huo?

Nchi zilizoingizwa kwenye mradi huu

Kwa mujibu wa taarifa za mradi huu wenye jina la 'Active Gene Drive Project in Africa,' kundi la kwanza unazihusi nchi za Burkina Faso, Uganda, Ghana, Cape Verde, Visiwa vya Sao Tome and Principe, Djibout na Tanzania

Swali la msingi wanalojiuliza wataalam ni hili; kwanini nchi ya Cape Verde imeingizwa kwenye mpango huu wakati nchi hiyo ilishatokomeza ugonjwa wa malaria?

Kama kweli lengo ni kumaliza mbu wa malaria tu, kwanini nchi isiyo na ugonjwa huo ipelekewe mbu wa kutengenezwa 'kuwala wale wa malaria?' Ukweli huu umewatia wasiwasi baadhi ya wataalam kwamba mradi huu ni mojawapo ya mipango inayofanywa kujaribu kupandikiza vinasaba vipya kwa Waafrika kwa malengo yasiyofahamika, au kutengeneza ugonjwa utakaolipuka baadaye.


Wanaotetea mradi huu wanasema haya ni majaribio ya kawaida na kwamba sehemu ya kwanza ya majaribio kama hayo ilifanyika nchini Marekani ambapo mbu hao walisambazwa kwenye majimbo ishirini.

Swali wanalojiuliza wataalam ni kama mbu waliosambazwa Marekani ndio haohao watakaosambazwa Tanzania au hawa wana malengo mengine?

Kumbuka mmoja wa wafadhili wakubwa wa mradi huu ni Taasisi ya Bill and Melinda Gates yenye makao yake makuu Seattle, Marekani. Hii ni familia ya matajiri zaidi duniani, ikiwa na ukwasi mkubwa unaoelezwa kufikia dola za Marekani bilioni 69 (sawa na shilingi trilioni 180 ).

Je, taarifa zitatolewa mapema?

Pamoja na IHI kueleza kuwa mbu hao hawatasambazwa, na kwamba huachiliwa tu kwa makundi ya ng'ombe




wanaoelekezwa kwao kwa ajili ya chakula, je, hakuna uwezekano wa "kujichanganya na kuingia" kwenye maeneo ya makazi ya watu?

Je, kuna mfumo wowote kwa wananchi kutoa taarifa kama ikitokea wamepata ugonjwa usiojulikana baada ya kuumwa na mbu hao.

Je, kuna mpango wowote wa kuandaa matibabu ya dharura au uangalizi maalum kwa wananchi watakaopata ugonjwa usiojulikana baada ya kuumwa na mbu hao.

Je, kuna utaratibu wa kutambua endapo kweli mbu hao wanafanya kazi wanayotakiwa (kuua mbu wa malaria tu) na siyo kudhuru mifugo au viumbe hai vingine.

Je, mbu hao wapya wanaweza kubadili jene zao baada ya kuachiwa.

Yako maswali mengine mengi ya kitaalam ambayo hayajatolewa majibu na au majibu yake yanaelekea kuwa ya ubabaishaji.

Ni muhimu sana serikali ya Tanzania ichunguze mradi huu kwa undani na ikibidi hata kutumia wataalam wengine wa nje wenye utaalam na vifaa vinavyoweza kubaini mengi katika kuendeleza mazalia ya mbu hao.



## Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

# Inakera msibani kugeuzwa jukwaa la siasa

KWA mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu, jukwaa ni sehemu iliyoinuliwa ndani ya jengo kubwa au katika uwanja, ambayo aghalabu hutumika kuonyeshea michezo, shughuli au kutolea hutuba.

Kwa mantiki hiyo, tunaweza tukawa na majukwaa mbalimbali katika jamii kama vile jukwaa la wanamichezo, jukwaa la elimu, jukwaa la wanasiasa, jukwaa la wanahabari, jukwaa la wakulima, jukwaa la wafanyabiashara, jukwaa la wahariri nakadhalika!

Msingi wa majukwaa haya umejengwa katika kuwakusanya watu kujadili, kubaini changamoto na kutafuta utatuzi wake, pamoja na mambo mengine.

Hata hivyo, inashangaza sana kuona taifa moja lenye zaidi ya watu milioni 60, makabila 120, wanaoelewana kwa kuzungumza lugha moja ya Kiswahili, ambao wako kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa kwa miaka 32 sasa, bado ni malimbukeni wa siasa.

Kutokana na haki ya kikatiba waliyopewa Watanzania ya kuwa na hiyari ya kujiunga na chama chochote, leo ni rahisi sana kukuta baba mwenye nyumba ni mwanachama wa CCM na mama mwenye nyumba yuko Chadema, achiliambali watoto na wapangaji kuwa kwenye vyama tofauti 19 vyenye usajili wa kudumu!

Kwa hiyo kunapotokea kifo cha mwanachama wa chama cha siasa, hasa mwanachama huyo akiwa pia kiongozi, utamaduni wa wafuasi kwenda msibani wakiwa kwenye sare rasmi za chama, hauna afya.

Wanawakwaza wafiwa kwa sababu pale ni msibani; mahala pa huzuni, tangu taarifa ya msiba mpaka wakati wa mazishi yake, siyo jukwaa la kuonyesha uwingi wao na jinsi wanavyosaidiana kisiasa!

Mfano, itakuwaje marehemu akiwa



*Mavazi ya CCM yakitawala mazishi*

kiongozi wa Chadema, baada ya kufariki mzazi wake ambaye ni kiongozi wa CCM, wafuasi wao wakija msibani wamevalia vyuo kutambulisha vyama vyao, hali itakuwaje? Ni vurugu!

Lakini, tunajisikiaje tunapokwenda na sare za vyama vyetu msibani na wakati mwingine vikundi vya vijana wa jumuia za vyama kuonekana ndiyo wabeba jeneza kwa kigezo tu aliyefariki alikuwa mkereketwa mwenzetu ilihali tulishindwa hata kupeleka msaada wa kibinadamu wakati mwanachama mwenzetu huyo akiugua hadi amekata roho?

Bado nawaza, bila utamaduni wetu wa kustahamiliana ingekuwaje wakati wafuasi wa chama hiki cha marehemu wakijimwambafai kwa bendera yao kufunika jeneza, na wale wa mfiwa ambao ni chama kingine cha siasa wakaja na sare zao wakilazimisha shughuli za msiba ule wasimamie wao kwa kuwa aliyefiwa ni kiongozi wa chama chao?

Tusingoje kushuhudia uvunjifu wa amani kutokea, nadhani tunahitaji sheria inayokataza kuvaa sare za vyama vya siasa msibani kama inavyozuiwa kuvaa sare hizo siku ya kupiga kura.

*Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546*

*Barua pepe:mtagaluka@gmail.com*

# Kenya

## Kalonzo tayari 'kuvaa viatu' vya Raila

**Na Julius MKAMBI**

KALONZO Musyoka ambaye kitaaluma ni mwanasheria, bado hajakata tamaa ya kutimiza ndoto ya kuwa Rais wa Kenya.

Tayari ameanza tambo na safari akidai yeye ndiye mwenye ufungo wa kumuondoa Rais William Ruto madarakani wakati uchaguzi mkuu utakapofanyika mwaka 2027.

Mwanasiasa huyu mwenye umri wa miaka 70, tayari ameshaanza kujipanga huku akisema anatumia mbinu aliyotumia Rais Ruto kushinda uchaguzi mkuu mwaka 2022.

Kalonzo alianza siasa mwaka 1983 alipowania kiti cha ubunge wa Kitui Kaskazini, lakini akashindwa, hata hivyo bahati ilimdondokea miaka miwili baadaye aliposhinda katika uchaguzi mdogo akiwa na umri wa miaka 32.

Mwanasiasa huyu ameshawahi kuhudumu nafasi ya Naibu Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Mambo ya Nje na pia Naibu Spika wa Bunge la Taifa, wakati wa utawala wa Rais Daniel arap Moi.

Pia aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa mara nyingine, na baadaye Waziri wa Mazingira ndani ya serikali iliyokuwa ikiongozwa na Rais Mwai Kibaki.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 uliogubikwa na ghasia pindi Rais Kibaki alipotangazwa kushinda kwa muhula wa pili na kuapishwa 'usiku,' ulisababisha kuundwa kwa serikali ya mseto na Kalonzo aliyemaliza nafasi ya tatu nyuma ya Kibaki na Raila Odinga, alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa 10.

Kalonzo ambaye mara tatu aliweka pembeni ndoto yake ya kuwa kiongozi wa Kenya na kuamua kumuunga mkono Raila, sasa anamtaka Raila kumuunga mkono katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2027.



*Kalonzo Musyoka*

Mwanasiasa huyo ambaye pia ni Kiongozi wa Chama cha Wiper, ambacho ni miongoni mwa vyama vinavyounda muungano wa Azimio One Kenya, amesema atawaokoa Wakenya kutokana na uongozi dhalimu na kusisitiza Rais Ruto ataweka rekodi ya kuwa rais aliyehudumu kwa muhula mmoja tu.

Raila anatajwa kuwa huenda akastaafu siasa za ndani ya Kenya endapo atapata nafasi ya kuwa ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika.

Miongoni mwa wanasiasa waliopo ndani ya Azimio la Umoja, Kalonzo ndiye anayeonekana mwenye uzoefu na tayari ameshaanza kujipenyeza kila pembe ya nchi akisaka kuungwa mkono. Huko anakopita, Kalonzo anajitambulisha kuwa ni mtetezi wa wananchi.

"Raila Odinga ni kiongozi wa chama. Naibu Kiongozi wa Azimio la Umoja One Kenya ni Martha Wangari Karua. Lakini, wakati Raila anaelekea Addis Ababa (mji mkuu wa Ethiopia), lazima tujipange. Niko tayari kuongoza upinzani katika nchi hii hadi tuikomboe Kenya," amesema Kalonzo katika moja ya mikutano yake.

Kalonzo amekua mstari wa mbele kumshutumu Rais Ruto huku akieleza kuwa katika kipindi chake, hali ya maisha imekuwa ngumu zaidi.

# Lembeli: Nilirudi CCM kwa kumwogopa Magufuli

**Na Mwandishi WETU**

JAMES James Daudi Lembeli, aliyewahi kuwa Mbunge wa Kahama, amesema aliamua kurejea Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kukiacha Chadema, kwa kumuogoa Rais John Magufuli.

Magufuli alikuwa rais wa awamu ya sita wa Tanzania, kuanzia Novemba, 2015 hadi Machi, 2021, alipofariki dunia.

Lembeli ambaye alikuwa mbunge kwa miaka 10, kuanzia 2005 - 2015, aliamua kuondoka CCM mwaka 2015 na kujiunga na chama cha upinzani, Chadema, kabla ya kuamua kurejea tena CCM, mwaka mmoja baadaye.

Amesema alihofia mengi, hata kuamua kurudi CCM, chama alichokiacha kwa madai kuwa "kilikuwa kimepoteza mwelekeo," hivyo alihitaji mbadala.

Mbunge huyo pia aliongoza Kamati ya Bunge iliyofanya uchunguzi wa tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu wakati wa Operesheni Tokomeza Ujangili ambayo iliwang'oa mawaziri wanne mwaka 2015.

Wiki iliyopita gazeti la Pambazuko lilimhoji Lembeli ambapo pamoja na kueleza woga wake uliomlazimisha kurejea CCM, pia amezungumzia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, uendeshaji wa bunge, muundo wa Muungano na masuala mengi.

**Swali:** Unazungumziaje hali ya kisiasa nchini?

**Jibu:** Pamoja na jitihada ambazo Rais Samia Suluhu Hassan amezichukua katika kipindi cha miaka mitatu kuwajengea wananchi kwamba yeye hapendi na hataki siasa za kibabe, wala chuki, sisi tulioko mitaani na hata vijijini; kwenye vijiwe vya kahawa, bado wananchi tuna shaka na msimamo wake.

**Swali:** Shaka zipi?

**Jibu:** Shaka zipo, hasa kwa uchaguzi ujao ambapo wagombea walio wengi hawakuwa chaguo la wananchi ndio maana viongozi wengi, hata wakiitisha



*James Lembeli*

mikutano, wananchi hawahudhurii na hali hii ni sehemu nyingi na kuficha hilo, aidha wanasomba watu kutoka sehemu nyingine au wanakusanya wanafunzi.

**Swali:** Kwa mtazamo wako unadhani uongozi wa Rais Samia unatekeleza kweli malengo yake?

**Jibu:** Ni vigumu kuyatekeleza yote katika kipindi hiki kifupi kwa kuwa hata ndani ya chama chake na katika serikali, wapo ambao mambo yake kadhaa, hawakubaliani nayo. Katika mazingira hayo, utekelezaji wa hayo yote ni mgumu.

**Swali:** Nini maoni yako kuhusu mabadiliko ya Sheria za Uchaguzi ambayo wapinzani wanalalamikia?

**Jibu:** Hili la mabadiliko ya sheria za uchaguzi, pamoja na kuwa ni hatua moja mbele kukidhi hoja na matakwa ya wananchi, halijaridhisha umma kwa mapana yake.

Maoni ya wananchi, wadau wa maendeleo na hata baadhi ya viongozi wa dini karibu yote hawajayapokea vyema. Wameyatupwa.

Naiona hatari mbele ya safari, viongozi wa dini pamoja na maoni yao kutozingatiwa, wamekaa kimya, nini maana yake, hii wanaweza kuja na kishindo kikubwa.

Kumbuka Waraka wa Maaskofu

*Inaendelea Uk. 12*

# Ana kwa Ana

## Lembeli: Nilirudi CCM kwa kumwogopa Magufuli

*Inatoka Uk. 11*

Katoliki, hawajaufuta uko majimboni, maparokiani, vingangoni na katika jumuia zao na bado unatumika kama rejea.

**Swali:** Kipi ulijifunza kipindi cha uongozi wa Rais John Magufuli?

**Jibu:** Kwanza kabisa, Rais Magufuli alikuwa rafiki yangu wa karibu. Aliumia sana nilipohamia Chadema, ndio maana hata alipofanya mkutano wa hadhara Kahama - wa kwanza baada ya yeye kuwa rais mwaka 2016, alinisihi nirudi, niondoke huko niliko.

Kwa kuwa mimi siyo mnafiki, aliponipa nafasi ya kusalimia nilimjibu hapohapo kwamba mimi bado ni Mtanzania, hivyo kwenda Chadema haikuwa dhambi na kwamba naweza kutoa mchango wangu kwa taifa.

Nilimwambia kwamba kurudi CCM siyo tatizo, lakini sababu zilizokuwa zimenitoa CCM, bado zilikuwapo na nilizitaja na kumuomba kusafisha kwanza nyumba yake kwa maana CCM, jambo ambalo alilifanya kadiri Mungu alivyomjaalia.

Lakini, pamoja na mazuri yake mengi, yapo ambayo kwa kweli yalitia doa mazuri yake. Alikuwa hashauriki, alichokiamini yeye ndicho ukimweleza kinyume chake, mnakosana au anakutumbua na mbaya zaidi hata kukudhalilisha.

Wapo viongozi wengi walitumbuliwa kwa kumbishia, alikuwa pia mkatili, na kwake sheria hazikuwa zinamuongoza katika kuendesha nchi.

**Swali:** Unadhani angekwepo Tanzania ingekuwa nchi ya aina gani leo?

**Jibu:** Angekuwapo leo, ni dhahiri udikteta ungekuwa umetamalaki na historia inakuambia udikteta huwa hauna maisha. Mifano hapa Afrika ipo mingi, Rais Idi Amini wa Uganda,Mfalme Bokassa Afrika ya Kati, Omar al Bashir -Sudan na wengineo.

**Swali:** Unadhani bado Katiba mpya inahitajika?

**Jibu:** Kama nchi inataka kuendelea kuwa na utulivu, amani na mshikamano, Katiba ni lazima. Pamoja na dhamira ya Rais Samia kuwa nzuri, naona kuna sheria zinatungwa sasa hivi kunyamazisha kilio cha Katiba, lakini sheria hizo zinakinzana na Katiba.

Kwa mfano tangazo la juzi la jina la Tume ya Uchaguzi kubadilisha Jina na kuwa Tume Huru ya Uchaguzi; ukisoma Katiba hata bila kuwa mwanasheria, hakuna kipengele cha katiba kinachotaja jina hilo la tume.

Hata sielewi wanasheria wanaomshauri Rais Samia kwa nini wanadhalilisha serikali yake kwa kushauri mambo kama haya?

**Swali:** Bado unaamini katika muundo wa serikali tatu katika Muungano wa Tanzania?

**Jibu:** Ni kweli, bado msimamo wangu ni uleule kwa sababu ndio suluhu ya matatizo yaliyopo kwenye Muungano, kwani bila seikali tatu, matatizo hayo hayataisha. Siyo hilo tu, ninaamni pia katika serikali ya majimbo hapa nchini.

**Swali:** Ni kitu gani kilikufanya ukarejea CCM?

**Jibu:** La kwanza ni uoga. Kipindi hicho kumkatalia Rais Magufuli ulikuwa unahatarisha maisha yako. Shahidi ni mama yangu mzazi alishuhudia hayo.

Sasa mzazi wako wa miaka 90 wakati huo anakuambia usubiri kwanza mimi nife ndio uendelee na misimamo yako hiyo. Katika mazingira hayo unafanya nini.

**Swali:**Unafikiri wanaosema kilichokupeleka Chadema ni Lowassa, je, wako sahihi? Maana aliporudi CCM na wewe ukarudi

**Jibu:** Hao wanaosema kilichonipeleka Chadema ni Lowassa, nawasamehe. Siyo kweli, narudia tena siyo kweli, ninaweza kuwaita ni machawa waliopitiliza.

Ukweli ni kwamba, nilitangaza kuhama CCM Julai 21 mwaka 2015 kabla ya uchaguzi wa kura za maoni ndani ya CCM

*Inaendelea Uk. 13*

# Lembeli: Nilirudi CCM kwa kumwogopa Magufuli

*Inatoka Uk. 12*

kwa wabunge. Lowasa na Khamis Mgeja walihamia Chadema baada ya jina la Lowassa kukatwa kwenye kinyang'anyiro cha urais na kunikuta mimi na Esther Bulaya (Mbunge) zamani tumejiengua CCM. Hao watu ninawasamehe, lengo lao ni kufanikisha uchawa wao.

**Swali:** Unauzungumziaje mwenendo wa Bunge la sasa?

**Jibu:** Bunge la sasa, kwa moyo wa dhati kabisa, siyo Bunge lililochaguliwa na wananchi. Hakuna ubishi labda mtu anataka kujifariji na kujifurahisha.

Kwa maoni yangu, Bunge la Samuel Sitta ndilo kwa kiwango kikubwa lililifanya kazi za wananchi.

**Swali:** Uliwahi kuongoza Kamati ya Bunge ya Operesheni Tokomeza Ujangili ambayo baadaye iliwang'oa mawaziri wanne, je ulikutana na vikwazo gani?

**Jibu:** Kwa kweli kwa kawaida mimi sijawahi kuwa na presha, lakini operesheni tokomeza nusura niondoke nayo kwa presha. Operesheni tokomeza iligubikwa na dhambi za kila aina, uonevu, dhuluma, wizi, mauaji na ufisadi wa kutisha.

Spika Anne Makinda aliponiteua kuongoza tume hiyo, mwanzoni niliamini haikuwa kazi ngumu kwa kuwa nilikuwa na uelewa mpana na maeneo ambako operesheni hiyo ilifanyika.

Kinyume chake tuliyoyashuhudia yalikuwa mazito kiasi cha muda wote wa zoezi kukosa usingizi kwa mapigo yangu ya moyo kwenda mbio. Vishawishi vilikuwa vingi pamoja na wajumbe wangu ambao walikuwa wanane.

Ripoti Ile ilitokana na hadidu za rejea ambapo kamati ilifuatilia kila malalamiko yaliyotolewa na mbunge wa eneo husika, kamati ilifika katika maeneo yote ili kubaini kama kulikuwa na ukweli au ya kutunga.

Hivyo, ripoti ile haikulenga mtu, bali kueleza ukweli wa kilichotokea. Ni kweli mwisho wa siku mawaziri wanne walipoteza nafasi zao.

Kuhusu vikwazo kama vilikuwapo, ni wazi ripoti ilipokelewa kwa mitazamo tofauti, wapo walioipokea kwamba ilikuwa wazi na wapo ambao waliiona imesababisha watu wao kupoteza nafasi zao.

Ukiacha watu wanaoitwa machawa, binafsi sijapata matatizo makubwa kutoka kwa mawaziri walioguswa na ripoti hiyo. Lakini nikiri kwamba nilipata matatizo hasa ya kisiasa.

**Swali:** Umekuwa ukichukizwa na ufisadi, unazungumziaje Ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali (CAG), ambazo zimekuwa zikionesha ubadhirifu lakini wahusika wamekuwa hawachukuliwi hatua?

**Jibu:** Niseme kwa kifupi tu kwamba tatizo hilo ni kubwa, ripoti hazijadiliwi, hatua hazichukuliwi dhidi ya watu wanaopora fedha na mali za umma.

Kwanini? Jibu ni mfumo wa sasa wa Bunge na siasa za sasa za nchi hii. Ndani ya Bunge hakuna mawazo wala fikra mbadala, bunge ni la chama kimoja.

Hakuna wa kumnyooshea kidole yeyote. Wahusika wengi ni watumishi wa serikali, serikali ni ya CCM, haiwezekani mbunge wa CCM ndani ya bunge kuinyooshea kidole serikali yake.

**Swali:** Nini matarajio yako katika uchaguzi mkuu ujao, je, utagombea tena jimbo ulilopata kuliongoza.

**Jibu:** Mimi namwombea Rais Samia ayaishi maneno yake na ahadi zake kwamba atahakikisha yaliyofanyika na kutokea mwaka 2019/20 hayatajitokeza tena.

Kinyume chake kuna dalili za kutokea ghasia. Watu sasa wameamka,wote tumuombe rais wetu ajae busara na hekima zimsaidie kutekeleza dhamira yake iliyojaa upako kuhusu uchaguzi wa baadaye mwaka huu na mwakani.

Kuhusu kugombea hapo mwakani, hilo nasubiri upako Utakavyoniongoza, nitatekeleza. Bado nguvu na uwezo upo.

# Makala

## Kauli ya 'maji ni uhai' inapopoteza maana

Na Pascal ADRIAN

MIONGONI mwa kero kubwa ambazo Watanzania wamekuwa wakipigia kelele tangu nchi ilipopata uhuru Desemba 9, 1961, ni matatizo ya kupatikana kwa huduma za uhakika za maji na umeme.

Hizi zimekuwa kero tangu wakati huo na zikaendelea kuwa kero hata baada ya kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar, 1964 na baadaye mwaka huohuo, Tanganyika kuungana na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania, bado wananchi wake wakaendelea kuwa na kero ya maji.

Kutopatikana kwa uhakika kwa huduma hizi muhimu, ndio kiu kubwa ya jamii yote ya Tanzania – kwani maji ni bidhaa muhimu mno katika kukamilisha maisha ya mwanadamu na viumbe hao, vitu vingine vinapaswa kufuata baadaye.

Kila mtu anafahamu kuwa maji ni uhai na umeme ni uchumi. Sasa tunaweza vipi kuendeleza uhai iwapo huduma za maji ni za kusuasua na tunawezaje kuendeleza uchumi wakati umeme haupatikani wa uhakika?

Haifai kutandaza mabomba ya maji kwa lengo tu la kuaminisha umma kuwa serikali ipo kazini na kwamba kero yao ya maji ya muda mrefu inaelekea kumalizika, na huenda maji yakapatikana kwa 'siku mbili-tatu, lakini kiongozi anayezindua mradi huo anapoondioka tu na maji yanakatika.

Siku kadhaa zilizopita, serikali ilizindua mifumo mipya miwili ya kudhibiti ukusanyaji wa ankara za maji ili kutatua malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi ya kutozwa kiasi kikubwa cha fedha tofauti na kiasi cha maji wanayoyatumia.

Rais Samia Suluhu Hassan alizitaka mamlaka za maji ziige mfano wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuweka mifumo itakayomuwezesha mteja



***Kijana akichota maji***

kutumia huduma ya maji kutokana na kiwango cha fedha anazolipia na pindi fedha zake zinapoisha, huduma itakatika mpaka atakapolipia tena.

Wazo la Rais Samia ni zuri na linafaa kupongezwa kwani litaondoa usumbufu wa ankara za kubambikiwa.

Hata hivyo, lipo jambo la kujiuliza hapa, je, hivi kero kwa Watanzania ni ukubwa wa ankara za maji au kupatikana kwa maji yenyewe? Nadhani suala la ankara linajitokeza kwa sababu linahusu fedha, lakini kimsingi wanacholalamikia watu wengi ni ukosefu wa maji.

Tena wakati mwingine utakuta kuwa huduma ya maji haipatikani, lakini mwisho wa mwezi ankara inaletwa ikiwa kubwa vilevile, kana kwamba watu wametumia maji.

Watu wanalalamikia ukubwa wa ankara kwa sababu wanaona wanaibiwa kwa kutakiwa kulipia huduma ambayo hawajaitumia.

Ni wakati sasa wa serikali, kupitia mamlaka zake, kuhakikisha kuwa kero ya huduma za maji, inamalizika na kuwapa wananchi kufurahia maisha yasiyokuwa na usumbufu wa kuwaza maji kila mara.

*Pascal Adrian ni mkufunzi katika Chuo cha Uandishi wa Habari cha DSJ, Dar es Salaam.*



Tangaza na

Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

# Makala

## Kudhibiti uhalifu mtandaoni kuzinufaisha nchi kiuchumi

**Na Mwandishi WETU, Arusha**

UHALIFU mitandaoni ni jambo kubwa. Unahusisha thamani kubwa ya fedha kiasi kwamba ukubwa wake – endapo utawekwa ndani ya nchi, unaweza 'kubeba' nafasi ya tatu kwa uimara wa uchumi duniani.

Wataalamu wanasema fedha za uhalifu huo zikiwekwa katika mizani ya uchumi, na kupewa nchi, basi nchi hiyo itakuwa ya tatu kwa uimara wa kiuchumi duniani, ikiwa na thamani ya matrilioni ya dola za Marekani.

Inaelezwa kuwa kiasi cha fedha kinachohusishwa na uhalifu mtandaoni kilikadiriwa kufikia dola za Marekani trilioni 8 mwaka 2023 na ifikapo mwaka 2025, kiasi hicho kitafikia dola trilioni 10.5.

Huu ni uchumi mkubwa ukitanguliwa na Marekani na China tu, kwa mujibu wa wataalamu wa masuala ya uchumi duniani.

Akiwasilisha mada katika kongamano la masuala ya uhalifu mtandaoni lilifanyika hivi karibuni jijini Arusha, Margus Magi, mtaalamu wa masuala ya mitandao kutoka Estonia, alisema kuwa watu wengi wanachukulia suala la uhalifu mtandaoni kama tishio, lakini nchi zikiamua zinaweza kunufaika nalo.

"Suala la uhalifu mtandaoni linachukuliwa kama hatari, lakini hatari hizo zinaweza kutumika kama kichocheo cha uchumi. Je, serikali ipo tayari kuzigeuza hatari hizo kuwa fursa," alihoji mtalaamu huyo katika kongamano hilo lililoandaliwa na Tume ya Tehama Tanzania.

Kwa mujibu wa Kampuni ya McAfee, uhalifu mtandaoni unakula kiasi cha asilimia moja ya pato la dunia kwa mwaka na kiasi hicho kikubwa cha fedha kikiokolewa kinaweza kuzisaidia nchi nyingi zinazoathiriwa na uhalifu mtandaoni.



Alisema kuwa utalaamu na vifaa vingi vya kudhibiti uhalifu mitandaoni ambavyo vinaweza kusaidia nchi kupunguza kiasi cha hasara inayopatikana kutokana na uhalifu mitandaoni.

Aliongeza pia kuwa biashara ya vifaa na utalaamu huo imekuwa ikiongezeka sana, hivyo nchi zilizojikita kufanya biashara hiyo zinanufaika pia.

Magi alisema serikali zitanufaika iwapo zitachukulia suala la kuendesha mambo yake kimtandao kama sehemu ya vipaumbele vyake.

"Vijana wengi leo wanatumia mitandao na wangependa kuona serikali zao nazo zikiendesha mambo kupitia mitandao ambako wao wapo. Pia wangependa kuona serikali ikiwa na ufanisi zaidi mtandaoni kama kampuni za Google au Netflix," alisema.

Alisema wakati umefika sasa kwa serikali kuacha kufikiria kwa urasimu na 'kujifunua' kwa watu ili huduma zitolewe kupitia mitandao.

Alisisitiza kuwa kwa kuwa watu wengi sasa wanaendesha maisha yao kupitia mitandao, na wangependa kuiona serikali yao ikiwapa fursa ya kufanya mambo yanayowaunganisha nayo mtandaoni, bila kulazimika kuwepo kwa urasimu usikuwa na maana.

Hivyo, akaishauri serikali kuwa sasa ni wakati wa kumfanya kila mtu atembee na serikali kiganjani kwake kwa kuwezesha

*Inaendelea Uk 17*

# Kudhibiti uhalifu mtandaoni

*Inatoka Uk. 16*

kupatikana huduma zote kupitia mitandaoni.

"Tusihofu kuhusu uhalifu mitandaoni kwani kama nilivyoeleza awali kuna njia nyingi za kukabiliana na suala hilo na pia uhalifu mitandaoni ni sehemu ya uchumi wa mitandao," alisema.

Magi alibainisha kuwa iwapo serikali ikiwekeza vya kutosha hakutakuwa na ulazima wa watu kufunga safari kwenda kufuata huduma katika majengo ya ofisi za serikali na hivyo kupunguza usumbufu.

Alisema mfumo huo utakuwa na manufaa manne makubwa ikiwamo uaminifu, kwani watu watakaopata huduma hawatakuwa na mashaka tena kuhusiana na huduma hiyo.

Aidha, mfumo huo utawezesha watu kupata muda mwingi wa kufanya shughuli nyingine huku ukikuza ari ya watu kufikiri.

Kwa upande mwingine, mfumo huo utawezesha watu kufikia serikali kwa urahisi na kuwapa nguvu wananchi kufanya yale watakayo kwa wakati watakao na siyo kusubiri huduma tu pale ofisi za serikali zinapofunguliwa.

Alisema baadhi ya huduma zinazoweza kutolewa mitandoni ni pamoja na kutoa ankara, kujaza fomu mbalimbali na kuzisaini, kutoa mishahara, usajili, kutoa risiti za malipo mbalimbali, malipo ya papo kwa hapo, ununuzi na kuandaa ripoti mbalimbali.

Akifunguia kongamano hilo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama, Dkt. Nkundwe Mwasaga, alisema serikali ipo tayari kuimarisha masuala ya mitandao kwani imeshaona faida zake.

Alisema mikutano kama huo waliouandaa ni chachu kubwa ya kuendelea kuhamasishana, kukumbushana na kubadilishana uzoefu na mawazo juu ya hatua stahiki ambazo zinatakiwa kuchukuliwa katika nafasi mbalimbali za kitaalam na kijamii.

"Katika ulimwengu wa sasa, mageuzi ya kidijitali ni nguzo kuu ya kuwezesha uchumi wa kidijitali," alisema.




"Mageuzi haya ya kidijitali yanajengwa na msingi wa dhana kuu mbili; kwanza ni kutumia teknolojia za kidijitali katika shughuli zetu ili kuongeza ufanisi, mapato na hata kukuza ubora wa bidhaa na huduma mbalimbali…

… Dhana ya pili ni mabadiliko ya tabia za binadamu yaani, hii inalenga kuhakikisha kuwa binadamu ambao ni watumiaji wa huduma za kidijitali na walaji wa huduma na bidhaa zitokanazo na Tehama, wanakuwa na utayari wa kuitumia ili kuleta mabadiliko na kuongeza ufanisi katika shughuli za kila siku."

Alisema dhana hizo mbili haziwezi kufanikiwa endapo mifumo ya kidijitali itatishia usalama wa nchi, itakuwa kikwazo kwa ukuaji uchumi, itatishia ukuaji wa biashara za kampuni na zile shughuli za mtu mmoja mmoja.

"Pia kutokuwepo kwa matumizi sahihi ya mifumo ya kidijitali kunaweza kusababisha kutwezwa kwa utamaduni wa taifa na utu wetu kwa kuruhusu taarifa za siri za serikali, kampuni na hata zile za mtu binafsi kupatikana kwa utaratibu usiokuwa sahihi na kutumiwa na watu wasiokuwa na dhamana ya kutumia taarifa husika….

… Hivyo, malengo ya mageuzi ya kidijitali hayawezi kufikiwa endapo suala la usalama wa mitandao linalowezesha matumizi salama ya huduma za kidijitali halitapewa uzito unaoendana na kasi ya maendeleo ya Tehama," alisisitiza.

# Michezo

## Mchakato wa mabadiliko Simba unachosha

Na Mwandishi WETU

IMEPITA miaka takribani minane sasa tangu klabu kongwe ya soka ya Simba kuanza mchakato wa kufanya mabadiliko ya uendeshaji wa klabu hiyo, lakini hakuna dalili ni lini mchakato huo utaleta ufanisi uliokusudiwa.

Lengo la kufanya mabadiliko hayo ni kuiimarisha klabu kwa kuifanya ijiendeshe kisasa zaidi. Hilo ni jambo zuri sana na ndio maana hata watani wao, Yanga, wakaamua kuiga.

Kinachostaajabisha, Yanga, ambayo ilianza mchakato huu miaka kadhaa baada ya Simba, inaonesha dalili ya kufikia mwishio mzuri, wakati Simba iliyoanza awali ikizidi kugubikwa na sintofahamu katika uendeshaji wake.

Ukiangalia namna klabu zote mbili zilivyotekeleza mchakato wa mabadiliko, unaweza kubaini pale ambapo Yanga wamefanya vizuri kuliko Simba.

Nadhani Yanga walitumia makosa ambayo Simba waliyafanya kwenye mchakato wao kama funzo na ndio maana wamefanya vizuri zaidi ya Simba hadi hivi sasa.

Lengo la mabadiliko haya lilikuwa ni kupata mwekezaji au wawekezaji kwa ajili ya kuendesha klabu, huku wanachama, ambao ndio wamiliki wa timu, wakiendelea kubakiwa na sehemu kubwa ya umiliki, lakini inaonekana Simba waliharakisha kumpata mwekezaji bila kufuata taratibu nzuri.

Simba waliharakisha kumpata Mohammed Dewji, maarufu kwa jina la MO akiwa mwekezaji, na inaelezwa kuwa akalipa fedha kwa ajili ya kununua asimilia 49 ya hisa za klabu, huku wanachama wakibakiwa na asilimia 51.

Lakini kinachoshangaza ni kuwa mwekezaji mwenye kiasi kidogo cha hisa ndiye ana sauti na mamlaka makubwa kuhusu uendeshaji wa klabu kuliko wanachama ambao wana kiasi kikubwa cha hisa.

Bodi ya Simba ipo mikononi mwa



*Mo Dewji*

mwekezaji ambaye ndiye anayeamua nani wa kuingia kwenye bodi hiyo kama mjumbe na mwenyekiti wake awe nani. Hii ni kasoro moja.

Bado kuna suala la kiasi cha uwekezaji uliofanyika. Wengi wanahoji jinsi thamani ya hisa 49 ilivyopatikana, kwani hakukuwahi kusikika ikifanywa tathimini kujua thamani ya Simba ni kiasi gani.

Ilikuja tu kutangazwa kuwa thamani ya asilimia 49 ya hisa ni shilingi bilioni 20. Hii ni kasoro nyingine.

Tena, wakati upande mmoja ukisema kuwa kiasi hicho cha fedha kilishalipwa na hivyo kumfanya Mohammed Dewji kuwa mwekesaji halali wa Simba, bado kuna wanaodai uthibitishio wa malipo hayo haujatolewa hadi leo. Hii inaweza kuwa ni kasoro nyingine katika mchakato huu wa mabadiliko.

Yanga wakajifunza katika kasoro hizo na ukiangalia mchakato wao, unaonekana kuwa utazaa matunda mazuri na mapema zaidi kuliko Simba iwapo Simba hawatataka kurudi mezani na kujipanga upya.

Yanga ilianza kwa kufanya tathmini ya jumla ya klabu ili kubaini matatizo yake ya msingi. Hapo wakawa wamefanya jambo kubwa kuelekea utatuzi wa tatizo – yaani kulifahamu tatizo lenyewe.

Wataalamu wanasema kulifahamu tatizo ndio hatua kubwa ya kwanza inayopaswa kufanyika kuelekea utatuzi wa tatizo hilo.

*Endelea Uk. 19*

# Mchakato wa mabadiliko Simba unachosha

*Inatoka Uk. 18*

Baada ya kulitambua tatizo wakatafuta ushauri kutoka ndani na nje ya nchi, kutoka kwa taasisi zenye uzoefu wa kuendesha vilabu vya soka kisasa kwa mifumo mbalimbali.

Wataalamu kutoka Ligi ya Hispania, Laliga wakaisaidia Yanga katika hilo kwa kuwaonyesha aina tatu za mifumo ya kuendesha vilabu ambayo wanaweza kuitumia na kufanikisha lengo lao.

Kati ya mifumo iliyopendekezwa na wataalamu hao, Yanga ikapendezwa na mfumo ambao utaleta wawekezaji (si mwekezaji), lakini wakati huohuo ukiwaacha wamiliki wa klabu, yaani wanachama, wakiwa na sauti kubwa katika klabu yao.

Inafahamika kuwa hakuna mwekezaji ambaye ataweka fedha zake kwenye mradi ambao thamani yake haijulikani. Ndio maana sasa Yanga imeajiri watu wahsusi wa kufanya tathmini ya thamani ya klabu.

Baada ya tathimini hiyo kukamilika ndio itajulikana hisa 49 ambazo zitauzwa kwa wawekezaji zina thamani gani.

Jambo jingine ambalo Yanga imelifanya vizuri kuliko Simba na kuwa na mfumo wa uongozi na utendaji ambao unaacha mamlaka na madaraka makubwa ya kiutendaji na uendeshaji wa klabu mikononi mwa mwenye hisa nyingi, yaani wanachama ambao watakuwa na asilimia 51 za hisa.

Chini ya mfumo mpya, Yanga itakuwa na taasisi tatu. Ukiacha klabu yenyewe kutakuwa na upande wa wawekezaji. Hawa wawili watakutanishwa chini ya kampuni mpya itakayoundwa mahsusi ambapo wawekezaji wakatakuwa na asilimia 49 ya hisa huku Yanga ikiwa na asilimia 51.

Ndani ya kampuni hiyo, kwa mujibu wa katiba ya Yanga, Rais wa Klabu ya Yanga (ambayo ni moja ya vyombo vitatu katika mhimili ya mfumo wa uongozi wa Yanga) ndiye atakuwa kiongozi mkuu wa bodi ya kampuni.

Hii imefanywa hivyo kwa sababu Yanga ndio itakuwa na hisa nyingi ndani ya kampuni, hivyo kwa mujibu wa taratibu za uwekezaji nchini, inapaswa kuwa na mamlaka makubwa katika bodi ya kampuni.

Wawekezaji watakaribishwa wengi, lakini ili mwekezaji apate haki ya kuwa na kiti kwenye bodi atalazimika kuwa na idadi fulani ya hisa alizonunua.

Unapozungumzia kununua hisa ina maana kuwa mwekezaji huyo atakuwa amelipa fedha inayolingana na thamani ya hisa hizo.

Haitaruhusiwa kwa hisa zote 49 kununuliwa na mwekezaji mmoja, kwa mujibu wa taratibu ambazo Yanga imejiwekea ni kuwa wanatakiwa takribani wawekezaji watatu ambao watakuwa na kiasi cha hisa ambazo kila mmoja atakuwa na haki ya kupata kiti katika bodi ya kampuni.


Kwa maana hiyo, haitatokea wakati wowote mwekezaji mmoja akawa na hisa nyingi kiasi cha kuipiku klabu katika umiliki wa kampuni.

Pia mfumo huo utaondoa uwekezani wa mtu mmoja kujimilikisha klabu na kuwaacha wanahisa wengi, yaani wanachama 'wakitangatanga.'



Nadhani Yanga wameonyesha njia nzuri katika mchakato huu, hivyo ni vyema Simba wakiri kuwa kuna sehemu wamejikwaa na siyo vibaya wakajifunza kwa watani wao ambao wanaonekana kwenda vizuri katika hili.

# Bata mzuri duniani...



*Mungu ana maajabu yake. Huyu ni bata. Hana rangi za kuchorwa wala kupakwa, ni aina ya bata wanaoitwa – "Bata wa Mandarin." Inaelezwa kuwa ndiyo bata wanaovutia zaidi ya wengine na kutajwa na taasisi mbalimbali duniani kuwa wanaongoza kwa uzuri. Wanapatikana Mashariki mwa India, na hufugwa na matajiri maeneo mbalimbali, hasa Marekani. (Picha na Shutterstock).*

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION